

ECO-SCHOOLS PROGRAMME - TANZANIA

KIONGOZI CHA MWALIMU KWA SHULE INAYOJALI MAZINGIRA NA ELIMU KWA MAENDELEO ENDELEVU Kwa Shule za Msingi Tanzania



Kimetayarishwa kwa ushirikiano wa
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili, Tanzania na
Danish Outdoor Council

ECO-SCHOOLS PROGRAMME - TANZANIA

**KIONGOZI CHA MWALIMU
KWA
SHULE INAYOJALI MAZINGIRA NA ELIMU
KWA MAENDELEO ENDELEVU
Kwa Shule za Msingi Tanzania**



Kimetayarishwa kwa ushirikiano wa
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili, Tanzania na
Danish Outdoor Council

Kimeandikwa: Elisa Pallangyo kwa niaba ya TFCG

© Tanzania Forest Conservation Group

Chapa ya Kwanza March 2017

Kimepigwa chapa: DTP

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya maandishi toka kwa TFCG

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania- Tanzania Forest Conservation Group (TFCG)

S.L.P 23410, Dar es Salaam-Tanzania.

Simu: 022 2669007,

Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz

Tovuti: www.tfcg.org

Kuhusu the Tanzania Forest Conservation Group

Kitabu hiki kimetengenezwa na Shirika la Kuhifadhi misitu ya Asili Tanzania (TFCG). TFCG ni shirika lisilo la kiserikali ambalo ujumbe wake ni kuhifadhi na kurudisha bioanuwai ya misitu muhimu kidunia ya Tanzania kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijayo.

YALIYOMO

SHUKURANI	2
1. Utangulizi	3
2. Elimu kwa Maendeleo Endelevu na muundo wa shule inayojali mazingira (eco-school)	3
Elimu kwa Maendeleo Endelevu (EME).....	3
Dhana ya Shule inayojali Mazingira (Eco-school)	6
Mtazamo wa Uchunguzi, Maono, Matendo na Mabadiliko (UMMM), IVAC..	13
Mbinu za kufundishia Elimu ya Mazingira	15
MATUMIZI YA ZANA ZA ELIMU YA MAZINGIRA	20
3. Uboreshaji mtaala	22
Uingizaji wa Elimu ya Mazingira katika mtaala	22
Mtazamo wa Haki Sawa na Shule inayojali Mazingira (Rights-Based Approach and Eco-Schools)	23
Uingizaji Miradi Midogo katika mtaala	25
4. Ushirikiano kati ya jamii na shule	29
Kufahamisha/pasha habari na kuhusisha	29
Kuhamasisha ukusanyaji / uwekaji pamoja rasilimali	31
5. Kuchangisha Fedha (Fundraising)	33
Utafiti unaohusu uchangishaji fedha	33
Rasilimali/mali za jamii	33
Watu wa kujitolea	33
Uongozi na majukumu katika uhamasishaji wa rasilimali	34
Miradi ya kuongeza kipato	34
Faharasa	36

JEDWALI

Jedwali 1: Mbinu na taratibu za kufundishia na kujifunzia.....	15
Jedwali 2: Uchambuzi wa taratibu za ufundishaji za Elimu ya Mazingira	17
Jedwali 3: Taratibu/mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, thamani na matumizi yake	19
Jedwali 4: Njia za kuifahamisha jamii juu ya elimu ya mazingira	30
Jedwali 5: Mpangilio wa kuomba ufadhili	35

SHUKURANI

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) linapenda kuwashukuru wote waliosaidia katika utayarishaji wa Kiongozi hiki:

- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuunga mkono kazi hii, kwa majadiliano na mapendekezo yao wakati ya maandalizi, hasa kwa Bwana Robert Lwikolela, Mratibu Elimu ya Mazingira;
- DOC (Danish Outdoor Council) kwa ushirikano wao katika kutengeneza Kiongozi hiki;
- DANIDA (Danish International Development Agency) kwa ufadhili wa kutengeneza Kiongozi hiki;
- Walimu katika shule za msingi zilizopo katika tarafa za Mvomero na Turiani, Wilayani Mvomero, kwa kutoa maoni;
- Waratibu Elimu wa kata za tarafa za Mvomero na Turiani kwa maoni wakati wa kuandika hiki kiongozi;
- Watumishi wa mradi wa AVA kwa kusaidia katika maandalizi ya kiongozi hiki hasa kwa Bwana Hassan Chikira, Meneja wa Mradi, Raymond Nlelwa, Hamisi Masinde, Emanuel Lyimo, Daniel Mwaifunga na Gerald Alphonce;
- Watumishi wa Ofisi ya Elimu wilayani Mvomero kwa majadiliano na ushauri wao muhimu wakati wa maandalizi ya Kiongozi hiki;
- Athman Mgumia kwa kuandaa michoro iliyopo katika kiongozi hiki;
- Elisa Pallangyo, Mratibu wa Programu kwa kuandaa Kiongozi hiki;
- Nike Doggart, Mshauri, TFCG kwa kusimamia uandaaji wa Kiongozi hiki;
- Charles Meshack, Mkurugenzi Mtendaji wa TFCG kwa kuunga mkono wakati wa maandalizi ya kiongozi hiki;

1. UTANGULIZI

Elimu ina uwezo wa kumpa binadamu maarifa na baadaye kumbadilisha mwelekeo na tabia yake kuendena na mabadiliko ya dunia.

Shirika la Kuhifadhi Mimitu ya Asili Tanzania pamoja na serikali ya Tanzania wamejitahidi kufanya kazi ya kujenga uwezo na welewa wa mazingira kwa shule, jumuiya na wananchi kwa ujumla ili waweze kutoa michango yao ya kuhifadhi na kulinda mazingira na rasilimali zao kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Mojawapo wa mbinu za kupata maendeleo endelevu ni pamoja na kutumia na kuendeleza Elimu ya Mazingira shuleni na katika jamii. Serikali imekuwa inaingiza Elimu ya Mazingira katika mitaala ya shule za msingi, sekondari na vyo. Uingizaji wa Elimu ya Mazingira katika mitaala itasaidia kwa kiasi kubwa kulinda na kuhifadhi mazingira yetu na hivyo kupata maendeleo endelevu.

Kiongozi hiki cha Mwalimu kinakusudia kuwapatia welewa, stadi na kuwajengea uwezo walimu wa kuingiza Elimu ya Mazingira na Elimu kwa Maendeleo Endelevu katika mtaala wa shule za msingi Tanzania. Kiongozi hiki pia kinamjengea mwalimu uwezo wa kutumia taratibu / mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazounga mkono Uchunguzi, Maono, Matendo na Mabadiliko (UMMM), IVAC. Mfumo wa UMMM unasisitiza kutumia njia za ufundishaji na ujifunzaji wa vitendo, kufikiri kwa makini, uhuru wa kujieleza/kulezea mawazo yako na kutumia mazingira yako kama zana za kufundishia na kujifunzia. Mbinu zote hizi zinaendeleza haki za binadamu na elimu bora kwa mwanafunzi.

Ni matumaini kuwa Kiongozi hiki kitamwezesha mwalimu aweze kuingiza Elimu ya Mazingira /Elimu kwa Maendeleo Endelevu katika mtaala na wanafunzi waweze kupata maarifa, stadi za maisha na njia sahihi za kubadilisha mwelekeo na tabia zao katika kufikia Maendeleo Endelevu.

2. MAENDELEO ENDELEU NA MUUNDO WA SHULE INAYOJALI MAZINGIRA (ECO-SCHOOL)

Matokeo

Mwalimu aweze kuelewa maana ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu, kuiingiza katika ufundishaji kwa kutumia mbinu za Shule inayojali Mazingira (Eco-schools) na kuzitumia vema kanuni za maendeleo ya uchumi, usawa kijamii na mazingira endelevu katika maisha

Elimu kwa Maendeleo Endelevu (EME)

Elimu ni utaratibu wa mafunzo ambao unamwezesha mtu kujijenga kiakili na kitabia. Kila Taifa lina mfumo wake wa elimu ambao unaweza kubadilika kutokana na malengo na mahitaji ya wakati uliopo. Elimu ni njia ya kusaidia na kuiwezesha jamii kukabiliana na changamoto za maisha sasa na baadaye. Elimu kwa Maendeleo Endelevu ni neno linalotumika zaidi kimataifa na lilianza kutumika katika waraka wa umoja wa mataifa uitwao Agenda 21. EME inawahimiza binadamu kujenga stadi, maarifa thamani na tabia ili waweze kutoa maamuzi ya jinsi ya kuishi kiendelevu.

Mwaka 2002 Umoja wa Mataifa uliamua 2005 hadi 2014 iwe karne ya Elimu kwa Maendeleo

Endelevu. Lengo hasa la UN ni kuweka mkazo katika juhudi za kukuza maendeleo endelevu duniani kwa kutumia elimu na ujifunzaji.

Maana ya Maendeleo

Maendeleo maana yake ni maendeleo ya watu. Mabarabara, majumba, kuongeza mazao, na vitu vingine vya aina hii, siyo maendeleo; ni vyombo vya maendeleo. Maendeleo yasiyokuwa maendeleo ya watu hayana maana kwani hayahusiani na maisha ya kesho tunayojenga (Nyerere Octoba, 1968).

Maendeleo ni mabadiliko chanya ya hali ya maisha ya jamii kutoka hali duni kwenda hali njema zaidi kwa kujitosheleza kwa mahitaji muhimu ya maisha ikiwemo chakula, malazi, mavazi na huduma bora za jamii zinazofanya jamii ipate maisha bora na ya furaha. Kwa mtu binafsi, maendeleo ni kuongezeka kwa ujuzi na uwezo, uhuru zaidi, ubunifu, nidhamu binafsi, wajibu na kujitosheleza kwa vitu (Rodney, 1972:9). Kwa ufupi maendeleo ni ustawi wa maisha ya watu. Kwa maana kwamba, watu wapate mahitaji muhimu ya kuishi kama chakula bora, maji, huduma bora za afya, malazi, elimu na huduma nyingine za kijamii. Mtu anayetembelea gari la kifahari wakati huohuo amekula chakula kisicho bora na kulala maeneo duni huku afya yake ikitererereka huyo hana maendeleo.

Maana ya Maendeleo Endelevu

Ili jamii iwe na maendeleo endelevu inahitaji kukidhi mahitaji ya sasa bila kuharibu au kuzuia vizazi vijavyo kupata na kukidhi mahitaji yao muhimu. Ni falsafa ya namna tunavyoweza kutumia raslimali zinazotuzunguka na kuhakikisha tunawarithisha watoto wetu rasilimali hizo bila kuzimaliza ili nao waweze kuendeleza maisha yao

Maana ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu

Elimu kwa maendeleo endelevu ni mfumo wa ufundishaji na ujifunzaji unaojikita katika mawazo na kanuni zinazoleta uendelevu. Mawazo hayo ni pamoja na haki za binadamu, kupunguza umaskini, maisha endelevu, amani, ulinzi wa mazingira, demokrasia, afya, bioanuwai, mabadiliko ya tabia nchi, usawa kijinsia, na ulinzi wa mila na tamaduni zetu. Katika shule zetu hatutaona njia za kujifunza na ufundishaji katika mitaala kwa ajili ya kuleta maendeleo tu lakini tutaona mifumo endelevu kama vile utawala, uhusishwaji wa wadau na jamii, mipango ya muda mrefu, ufuatiliaji na upimaji.

Kuhusisha mtizamo wa shule nzima, itamaanisha shule yote ikiwa ni pamoja na wanafunzi, walimu na watawala watafanya kazi kujenga shule endelevu ambazo Elimu kwa maendeleo endelevu itaingizwa katika mitaala.

Uingizwaji wa elimu kwa maendeleo endelevu katika shule haitaongeza tu uhifadhi wa mazingira vizuri pekee lakini ukitekelezwa vizuri utaongeza ubora wa elimu na njia endelevu za kuishi.

Kwa nini maendeleo endelevu ni muhimu?

Watu zaidi ya bilioni moja duniani wanaishi katika maisha ya ufukara. Watu chini ya asilimia 20 ya idadi ya watu duniani hutumia zaidi ya asilimia 80 ya rasilimali za dunia.

Malengo makuu ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu

Elimu kwa maendeleo endelevu ina lengo ya kusaidia watu kujenga mwelekeo, stadi na maarifa ili kujenga maamuzi kwa ajili ya wao wenyewe na wengine kwa sasa na baadaye na

kutenda kutokana na maamuzi waliyoyafanya. Inamaanisha siyo tu kuwapa watu habari bali kuhakikisha kuwa shule zinaelekezwa kubadilisha jamii kuelekea matendo endelevu.

Malengo ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu

- Kujenga welewa wa maana ya maendeleo endelevu.
- Kuhakikisha kuwa maarifa ya Elimu kwa maendeleo endelevu yanatolewa na kutumiwa kwa vitendo katika ngazi zote za elimu (formal education).
- Kuimarisha maarifa, welewa na uhusishwaji wa walimu na wakufunzi katika maana na dhana ya maendeleo endelevu ambapo kwa pamoja huhusisha uhusiano wa uchumi, mila, siasa na tamaduni.
- Kuchanganua na kuchambua thamani ya maana mbalimbali za maendeleo endelevu.
- Kutengeneza kivyako maana ya maendeleo endelevu.
- Kutengeneza ubia kati ya wadau ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.
- Kuunda mfumo ambapo Elimu kwa maendeleo endelevu inaweza kukuzwa na kuendelezwa.

Wajibu wa Elimu katika Maendeleo Endelevu

Elimu ni muhimu katika kukuza thamani, tabia na mienendo ya maisha inayohitajika katika maisha endelevu. Elimu inahitajika katika kukuza welewa, kuisaidia jamii, watu binafsi na serikali ili kuweza kutoa maamuzi sahihi. Elimu haitoi tu habari lakini inawajenga watu katika matendo endelevu.

Uhusiano kati ya elimu na maendeleo endelevu

Elimu ni ufunguo wa uwezo wa kufikia matarajio endelevu kwa taifa lolote

Elimu inaweza:

- Kuongeza mazao ya kilimo.
- Kupunguza idadi ya vifo.
- Kuwafanya wanawake kutoa maamuzi sahihi.

Kusudi la elimu kwa maendeleo endelevu

Kufundisha na kujifunza kwa ajili ya maisha endelevu ya baadaye itakuwezesha mwalimu kupanga uzoefu wa ujifunzaji ambao utawafanya wanafunzi kujenga na kutathmini njia mbadala kwa ajili ya maisha ya baadaye ambayo ni endelevu na kushirikiana na wenzao ili kujenga ndoto zao za dunia nzuri kufikiwa.

Ngazi za maendeleo endelevu

- Mazingira: Welewa wa utajiri wa maliasili zetu na udhaifu na uendeleo wa mazingira yetu.
- Uchumi: Unyeti na umuhimu wa ukuaji wa uchumi na athari/matokeo yake kwa jamii na mazingira.
- Jamii: Welewa wa taasisi za kijamii na wajibu wao katika mabadiliko na maendeleo ya tamaduni zao.

Sehemu za elimu kwa maendeleo endelevu

- Maarifa
- Stadi / ujuzi
- Taswira
- Thamani

Elimu kwa Maendeleo Endelevu hutetea yafuatayo:

- Kujifunza kwa kutumia njia na mbinu anuwai kwa pamoja ambazo huingizwa katika mtaala na sio somo moja tu kwa ajili ya kuleta **Elimu kwa Maendeleo Endelevu**.
- Kushirikisha thamani na kanuni zinazozungumzia maendeleo endelevu.
- Fikira yakinifu na utatuzi wa matatizo ambazo huongeza kujiamini katika kutatua matatizo na changamoto za maendeleo endelevu.
- Ufundishaji anuwai.
- Wanafunzi kushiriki katika maamuzi ya jinsi ya kujifunza.
- Kutatua matatizo ya taifa na kimataifa na kutumia lugha ambazo wanafunzi hutumia zaidi.

Dhana ya Shule inayojali Mazingira (Eco-school)

Utangulizi: Dhana ya Shule inayojali Mazingira ilibuniwa nchini Denmark mwaka 1994. Ni mojawapo ya programu ambazo zinaendelezwa na *Foundation for Environmental Education (FEE)* ambayo imeenea katika nchi nyingi duniani.

Maana ya Shule inayojali Mazingira

Ni shule ambayo inazingatia sera ya mazingira katika kuongoza shughuli zake ambazo zinafuata ngazi saba ambazo huruhusu shule ijulikane kama shule inayojali mazingira na hivyo kuitwa Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*).

Dhana ya *Eco-school* imejengwa kutokana na kuweka mazingira katika kitovu cha ujifunzaji shuleni. Mazingira yamepewa kipaumbele katika mtaala na katika shughuli za kila siku. Mambo yahusiyo mazingira huweza kuchukuliwa katika mtaala na kufanyiwa kazi katika shughuli na changamoto za kila siku shuleni na nyumbani pia. Dhana hii hukazia matendo na uwezo, uhamishaji wa maarifa, ujuzi na thamani kwa kutumia ushirikiano wa shule na jamii.

Shule inayojali Mazingira (Eco-school) na maendeleo endelevu

Shughuli ya Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*) sio tu kufanya shule ipendeza kimazingira bali zaidi inatakiwa kuwajengea walimu, wanafunzi na jamii inayoizunguka shule uwezo, maarifa ya matumizi endelevu ya maliasili ili waweze kuongeza ubora wa maisha yao.

Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*) ni zaidi ya usimamizi wa mazingira shuleni. Ni program ya kukuza welewa wa mazingira unaohusishwa na masomo yote yaliyoko katika mtaala. Zaidi ya hapo, masuala mtambuka kama vile; elimu kwa maendeleo endelevu, kupunguza umaskini, ujasiriamali, haki katika mazingira na jamii, elimu ya afya yote haya yanaweza kutatuliwa kwa kuhusisha *Eco-schools*.

Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*) ni mkakati wa demokrasia na ushiriki unaotoa fursa kwa wajifunzaji (shuleni na wanajamii) ili waweze kujizoeshwa uraia wao katika maeneo yao.

Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*) ni mchakato wa ujumla unaofanya kazi kwa kuhusisha shule nzima pamoja na jamii inyoizunguka shule na vyombo vya habari. Inahamasisha kazi kwa pamoja (teamwork), na hujaribu kushirikisha welewa anuwai katika kuendesha shule katika mbinu za kuendeleza na kukuza usimamizi wa mazingira, maendeleo na uendelevu.

Eco-schools na Elimu kwa Maendeleo Endelevu

Mfumo wa Shule inayojali Mazingira (*Eco-schools*) unaonyesha vichocheo muhimu vya elimu kwa maendeleo endelevu (ESD) ambavyo ni:

- (a) Kukuza na kuongeza ubora wa elimu.
- (b) Kuelekeza mfumo wa elimu uliopo katika ngazi zote ili uweze kushughulikia maendeleo endelevu. Kutoa elimu inayofaa ambayo inajumuisha kanuni, ujuzi, taswira na thamani endelevu.
- (c) Kukuza welewa wa jamii juu ya uendelevu kwa kutumia shughuli hisishi (sensitization activities).
- (d) Kuwafunza wafundishaji wa ESD kama vile kufundisha juu ya uanzishwaji wa miradi midogo, uingizwaji wa mazingira katika mitaala n.k.
- (e) Kuwahusisha wadau mbalimbali katika shughuli za elimu, ambao ni pamoja na serikali ya Tanzania, sekta binafsi na asasi zisizo za kijamii katika uanzishwaji wa miradi midogo (micro projects).

Programu ya Eco-schools nchini Tanzania:

Programu ya Shule inayojali Mazingira hapa nchini inakusudia: kukuza kanuni za elimu kwa maendeleo endelevu nchini Tanzania kupitia shule za msingi na kukuza ushirikiano wa shule na jamii katika matumizi endelevu ya maliasili kwa kuongeza faida kwa wanafunzi wanaotoka katika shule maskini na jamii zinazoizunguka shule.

Eco-schools na uwezo wa wanafunzi

Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*) huongeza uwezo wa:

- Mawasiliano kwa ajili ya kukuza majadiliano kati ya walimu na wanafunzi na kati ya wanafunzi wenyewe
- Kutengeneza maono, kuona mbali (vision)
- Kufikiri kwa makini
- Kutengeneza taswira mpya
- Kutoa maamuzi
- Kufanya matendo sahihi

Hatua 7 za Kuunda Shule inayojali Mazingira

Hatua saba za kuunda shule inayojali mazingira (*Eco-School*) zinatambuliwa kimataifa, hata hivyo mpangilio na jinsi ya kuzitumia hutegemea na eneo lenyewe.

1. Kuunda kamati ya Eco- School. Kamati hii inaundwa na:

Ndugu wajumbe, kazi yetu ni kupanga, kusimamia, kutathmini shughuli za mazingira na kushirikisha jamii katika utunzaji wa mazingira



- Mwakilishi 1 kutoka Kamati ya Shule
- Wawakilishi 2 wa wazazi
- Walimu 2
- Wanafunzi 4
- Mwalimu mkuu

2. Tathmini ya mazingira ya shule

Wajumbe, kama mnavyoona kuchanganya taka zinazooza na zisizooza ni hatari kwa mazingira, itabidi tutafute ufumbuzi haraka.



- Angalia changamoto zilizoko shuleni kutokana na idadi, ubora, na upatikanaji wa rasilimali na athari za uharibifu wa mazingira shuleni na katika jamii
- Tabia na matendo ya watu
- Njia za kupatia kipato, uwekaji akiba/dunduiza na matumizi

3. Kutengeneza maono na malengo

Maandiko malumu yanayoelezea shule itakavyoshughulikia changamoto zilizogundulika wakati wa ukaguzi wa mazingira

4. Kutengeneza Mpango Kazi




- Orodhesha shughuli, hatua za kuchukua, nani mhusika na muda wa kufanya shughuli.
- Huongoza utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.
- Huwezesha kutekeleza malengo.
- Ni zana/kifaa cha kupimia uwajibikaji.

5. Kuhusisha mtaala (localize curriculum) kwa:



- Kutumia taratibu mahsusi za ufundishaji
- Kutumia zana zinazopatikana katika mzingira yetu
- Kuwepo kwa tathmini ya kila wakati (continuous assessment)

6. Ufuatiliaji na upimaji shughuli za Eco-school



- Pitia/angalia maendeleo ya program
- Andika maendeleo yaliyofikiwa na changamoto za program
- Tembelea mara kwa mara shughuli za program
- Changanua/chunguza mpango kazi, shughuli baada ya shughuli
- Tathmini matokeo ya program kwa walengwa
- Husisha matokeo ya tathmini katika shughuli

7. Kujulisha na kuhusisha jamii kubwa kwa kutumia:

Baba umeona somo la upandaji wa miti ya matunda katika jarida la MAZINGIRA?



- Barua pepe
- Mbao za matangazo
- Redio
- Mabaraza
- Mikutano
- Ripoti za shule
- Muziki
- Drama
- Siku za wazazi (open days)

Shughuli za kufanya

Wanawarsha wafanye yafuatayo:

Shughuli ya 1: Kueleza maana ya Maendeleo Endelevu

Swali la 1: Taja changamoto 3 za maendeleo endelevu katika wilaya yako

1.
2.
3.

Swali la 2: Taja matatizo ya maendeleo endelevu katika wilaya yako na taifa na uoanishe yanayofanana na yaliyo tofauti

Yanayofanana:

1.
2.
3.

Yaliyotofauti:

1.
2.
3.

Swali la 3: Ni wapi katika mtaala wanafunzi hujifunza mambo ya dunia kuhusu:

Jambo

1. Idadi ya watu
2. Usalama wa chakula
3. Makazi mijini
4. Nishati
5. Viwanda
6. Spishi
7. Mabadiliko ya tabianchi

sehemu katika mtaala

-
-
-
-
-
-
-

Shughuli namba 2 - vipimo vya Maendeleo Endelevu

Swali la 1: Kwa nini kipimo cha siasa kwa maendeleo endelevu ni kipengele muhimu?

Shughuli namba 3 – Tafakari

Swali la 1: Andika vitu 5 ambavyo vinatakiwa viwepo katika maana ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu

1.
2.
3.
4.
5.

Swali la 2(a) Kwa kutumia hivyo vitu 5 andika kivyako maana ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu.

Swali la 2(b) Kwa fikra zako mwenyewe je nini maana ya elimu kwa maendeleo endelevu?

.....

Swali la 2 (c) Unawezaje kutumia maliasili zilizoko katika eneo lako kufundisha na kujifunzia juu ya maendeleo endelevu ya binadamu?

Shughuli namba 4

Swali la 1: Je ni shughuli gani unaweza kuzifanya kuongeza welewa wa jumiya ya shule nzima kuhusu umuhimu wa elimu kwa maendeleo endelevu katika shule yako?

Mtazamo wa Uchunguzi, Maono, Matendo na Mabadiliko (UMMM), IVAC

Kusudi: Kuwawezesha/kuweka wazi mtazamo wa dhana ya (UMMM) IVAC kwa walimu

Matokeo ya ujifunzaji: Baada ya mafunzo ya eneo hili walimu wataweza

- Kuelezea mtazamo wa UMMM kwa wanafunzi.
- Kutumia mtazamo wa UMMM katika kujifunzia na kufundishia.
- Kuanzisha miradi midogo kwa kutumia mtazamo wa UMMM.

Uwezo wa ujifunzaji:

Baada ya eneo hili walimu wataweza:

- Kuulizia na kugundua matatizo ya mazingira
- Kuwa na mtazamo wa matatizo ya mazingira na shida zilizoko
- Kujenga maamuzi sahihi juu ya masuala ya mazingira na miradi midogo
- Kutenda matendo sahihi
- Kufanya tafiti zinazohusu mazingira

Mtazamo wa UMMM ni mtazamo muhimu sana katika kufundishia na kujifunzia unaotumika na *Eco-schools* katika kutekeleza elimu ya mazingira kwa ajili ya uendelevu.

Ni mtazamo wa kujifunzia/kufundishia ambao unajumuisha mitazamo shirikishi mingine.

Mtazamo wa UMMM

Ni mtazamo shirikishi na ambao unamlenga zaidi mwanafunzi katika kufundishia na kujifunzia.

Mtazamo huu (UMMM) unasisitiza njia za kufundishia na kujifunzia ziwe za matendo na kutumia mazingira ya asili. Mtazamo huu unasisitiza wanafunzi kufikiri kwa makini na kuelezea mawazo na mitazamo yao katika uhalisia wa maisha kwa kuongozwa na mwalimu. UMMM hupelekea kuendelea ujuzi wa maisha na thamani za watu binafsi ambazo ni muhimu kwa maisha na maendeleo ya jamii. Katika elimu ya mazingira, wanafunzi huchunguza, huelezea maono yao, huelekeza jinsi ya kutenda na mabadiliko kutokana na jinsi walivyoelewa na mahitaji ya mazingira yanayogusa maisha yao.

Faida za mtazamo wa UMMM

- Hushawishi wanafunzi kila wakati kuchunguza dhana wanayofundishiwa na kujifunzia.
- Wanafunzi wanauliza maswali muhimu kila wanapofundishwa dhana na vipengele.
- Wanafunzi wanajibidisha kutafuta majibu ya maswali wanayoulizwa/kukutana nayo.
- Kila wakati wanafunzi hutafuta faida na hasara za majibu wanayopewa.
- Wanafunzi hutafuta maono na kupata mapendekezo.
- Wanafunzi hujifunza jinsi ya kujieleza wenyewe.
- Mtazamo huu hutumainisha wanafunzi kujifunza



wenyewe katika matukio na ugunduzi.

- Huusisha mafunzo darasani na mazingira yahusiyo jamii zinazozunguka shule.
- Inatumainisha wanafunzi kufikiri kwa makini.
- Inatumainisha wanafunzi kushiriki katika mchakato wa kufundishia na kujifunzia.
- Mtazamo huu huwafanya wanafunzi kutambua vyema mazingira na maliasili zake.
- Husaidia wanafunzi kutambua matatizo ya mazingira na mbinu za kuyakabili.
- Hutumainisha wanafunzi kupendekeza njia za kutatua matatizo ya mazingira na mchakato wa mabadiliko.

Mbinu za kuuliza maswali ya kuongeza / zidisha UMMM

Uchunguzi: Uchunguzi unaelekezwa na maswali yafuatayo

Ni kwa nini ni muhimu kwetu?

Je aina ya maisha na hali tunayoishi hutengeneza ushawishi?

Je zamani ilikuwaje na kuna mabadiliko yoyote?

Je itakuwaje mbeleni kama hakuna lolote litakalofanyika kubadili huu mwenendo?

Maono:

Kuna njia gani mbadala ambazo tunafikiria?

Je kuna hali gani katika nchi na tamaduni nyingine?

Tunapendelea nini na kwa nini?

Matendo:

Kuna uwezekano wa matendo gani ya kuweza kufikia mabadiliko?

Je ni matendo gani ya kufanya?

Mabadiliko:

Mabadiliko gani yatatuleta karibu na maono?

Mabadiliko katika maisha yetu, darasani na katika jamii?

Matumizi ya mtazamo wa UMMM

Matumizi ya mtazamo wa UMMM yanaweza kuelezewa kwa kufikiria dhamira ya elimu ya mazingira kama vile MAJI, USIMAMIZI WA TAKA, MISITU, NISHATI na mengineyo.

Maswali elekezi:

Je kuna vyanzo vipi vya maji katika mazingira yako?

Vyanzo vya mito vinapatikana wapi katika jamii yako?

Ubora wa maji ulikuwaje miaka kumi iliyopita na ukoje sasa?

Ni kwa nini ni muhimu kulinda vyanzo vya maji katika jamii?

Ni muhimu kila baada ya uchunguzi wa chochote katika mazingira au dhana, ifuatiwe na ripoti ya yaliyogundulika na majumuisho.

Sehemu nyingine ya UMMM ni maono ambapo maswali elekezi yanaweza kuwa:

Kama mwanafunzi ninataka mchakato wa usimamizi wa taka uwe wa namna gani katika jamii?

Sisi kama watoto tunawezaje kusimamia takataka tofauti na watu wazima?

Usimamizi hafifu wa taka utatuathiri vipi sisi watoto?

Matendo na mabadiliko kama sehemu ya elimu ya mazingira yanaweza kutumiwa na walengwa kwa kushawishi matendo yatokanayo na wadau kutoka shule na jamii.

Mfumo wa matendo unaweza kutekelezwa kwa kutumia mtu mmoja mmoja, vikundi, au jamii kwa kutumia uongozi mbalimbali kupitia meseji, drama, majadiliano. Wanafunzi wanaweza kuhusika kwa kuwapelekea ujumbe jamii kupitia redio, maandiko, video na mikutano ya wazazi.

Shughuli ya kufanya:

Jiweke kwamba unafundisha darasa la sita juu ya vitendo na shughuli zinazohatarisha misitu katika mazingira yao (Jiografia drs la 6 Mada kuu/mada ndogo: 2.4 Misitu; Tumia mtazamo wa IVAC katika kufundisha kipindi kwa vitendo)

Mbinu za kufundishia Elimu ya Mazingira

Matokeo ya mafunzo

Hadi mwisho wa kitengo hiki ninategemea

- Kukubali (adopt), kutafiti, kuimarisha na kutumia njia sahihi mbalimbali kufundishia elimu ya mazingira
- Elezea kwa ufasaha taratibu tofauti, mazingira na stadi za kuwapatia wanafunzi moyo wa kuhifadhi mazingira

Uwezo

- Kutambua mbinu anuwai ambazo zinaweza kutumika kufundishia elimu ya mazingira
- Elezea njia sahihi kwa kila utaratibu iliyotambuliwa
- Kuoanisha yaliyomo katika taratibu sahihi

Mada: Mbinu za kufundishia elimu

Jedwali 1: Mbinu na taratibu za kufundishia na kujifunzia

Utaratibu	Jinsi ya kufanya/Shughuli
Majadiliano	Maswali na majibu, mjadala, kuelezea hadithi, mahojiano, safari za mafunzo (field visit), bungua bongo
Drama	Michezo ya kuigiza, drama, mazungumzo, mjadala
Maonyesho (exhibition)	Maonyesho, maelezo kwa kutumia picha, chora ramani juu ya ardhini, ramani ukutani, vitu halisi
Uwakilishi	Michoro, chati, picha, mabango
Utaratibu wa vikundi	Kuripoti, kukaa katika vikundi, bungua bongo (brainstorming)
Utatuaji matatizo	Ushindanishaji, uchambuzi, mafumbo
Kudadisi na uvumbuzi	Kazi za miradi, utafiti, safari za mafunzo, maswali, kudadisi na uvumbuzi, mahojiano
Ujifunzaji wa ushirika	Majadiliano, kurekodi, maswali na majibu, kuripoti
Utaratibu wa miradi	Kutumia vikundi,
Michezo ya uigizaji (role play)	Dhihirisha, elezea, kuhusianisha, dhanja
Kutafsiri picha	Kuangalia, husianisha,
Cinema	Kuonyesha, kuoanisha
Jaribio	Kutoa maagizo, kuangalia, kurekodi, kuripoti, kuandika
Ugunduzi wenye mwongozo	Kutoa maelezo, kuelezea, kusoma, safari za mafunzo, utafiti

Katika eneo hili mwalimu atawezeshwa kuelewa mbinu sahihi za ufundishaji ambazo

zitawawezesha wanafunzi kupata uwezo wa kiutendaji ambao utachangia katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Eneo hili litawawezesha kuelewa maana ya:

Mazingira: Mazingira ni vitu vyote vihusivyo mazingira katika mazingira na kwa ajili ya mazingira

Taratibu / mbinu za elimu ya mazingira: Ni mikakati na vitendo vya namna ya kutatua matatizo na changamoto zitokanazo na shughuli za binadamu

Utambuzi wa mikakati utakufanya kupata maarifa, ujuzi, maono, mtizamo na kubadilika kwa tabia na kuchukua hatua juu ya matumizi, ulinzi, na matumizi endelevu ya maliasili.

Maswali ya tafakari

- Neno mazingira lina maana gani kwako?
- Kwa nini umehusishwa katika kipengele hiki?
- Ni utaratibu gani wa ufundishaji katika kitengo hiki ambao umeshawahi kuutumia?
- Ni taratibu zipi ambazo haziwezi kutumika katika elimu ya mazingira?

Jedwali 2: Uchambuzi wa taratibu za ufundishaji za Elimu ya Mazingira

Taratibu / mbinu	Unachohitaji	Jinsi ya kufanya	Faida	Hasara
Mahojiano	Unahitaji kujua kama mahojiano yatakuwa katika vikundi au la, kati ya walimu na wanafunzi au katika jozi za wanafunzi	-Uisome na ujue mada vizuri -uwe na uamuzi juu ya mbinu za kutumia -andaa jinsi ya kutathmini mchakato wa kipindi chako -waongoze jinsi ya kuripoti na jitahidi kuwahusisha ambao hawana uwezo mkubwa	-Ni utaratibu ambao huwashirikisha/huwahusisha wanafunzi -wanafunzi huelewa vizuri wakihusishwa -mwalimu huweza kuwaelewa wanafunzi wake kiwelewa na uwezo -humwezesha mwalimu kuongeza nukuu zake kwani nyingine hakuwa nazo -huongeza kujiamini kwa mwanafunzi zaidi	-Kama haikutayarishwa vizuri wanafunzi wengine hushindwa kushiriki - wanafunzi werevu zaidi huwafunika wengine wasionekane -uchaguzi wa mada usipoangalia wanachofahamu wanafunzi, utaratibu huu hufeli
Kazi za vikundi	-Karatasi za kuandikia za kila kikundi -Uwe na maamuzi ya jinsi ya kuunda kikundi	-Usome na uwe na welewa wa kazi yenyewe -Utayarishhe kazi ya/za kuwapa vikundi -waweke wanafunzi katika vikundi -wape wanafunzi maelezo -waongoze	-Ni mbinu/utaratibu shirikishi -stadi kama vile uongozi hupatikana -wanafunzi wanapata uwezo wa kulinganisha walichokuwa nacho	Kama hakuna maandalizi na mwongozo mzuri wanafunzi wenye uwezo zaidi huwafunika wasio na uwezo
Maonyesho	-Vitu vya kuonyesha -weka maelezo yakutosha katika kila unachoonyesha -maarifa ya kitakachoonyesha yanahitajika kabla ya maonyesho	-Fundisha maudhui (content) ya lazima -ainisha kinachotakiwa kuonyeshwa -waongoze wanafunzi kutengeneza watachaoonyesha	Wanafunzi wanashirikishwa	-Kufanikiwa kwake hutegemea uwezo wa mwalimu -Kufanikiwa kwake hutegemea vitu vilivyoko vya kuonyesha

Taratibu / mbinu	Unachohitaji	Jinsi ya kufanya	Faida	Hasara
Ugunduzi	<ul style="list-style-type: none"> -Kufikiria kwa makini sehemu ya kutembelea -Andaa madodoso -Andaa kalamu na mahali pa kuandika matokeo (daftari n.k) 	<ul style="list-style-type: none"> -Tayarisha kazi vizuri -Tayarisha maswali yatakayotumika -Tembelea eneo husika kabla -Elezea jinsi ya kufanya na jinsi ya kuripoti 	<p>Wanafunzi wanagundua habari wenyewe na sio rahisi kusahau</p>	<ul style="list-style-type: none"> -Mbinu hii huitaji mwalimu mwenye kujitumana mwenye uwezo na mwenye welewa. -Inahitaji muda wa kutosha
Safari za mafunzo	<ul style="list-style-type: none"> -Tembelea eneo lengwa kabla -Welewa wa mada husika ni muhimu -Eneo liwe na maudhui (content) ya kutosheleza 	<ul style="list-style-type: none"> -Maandalizi ya kipindi -Tembelea eneo husika -Wape wanafunzi maelezo ya kutosha ya kitu/vitu/shughuli ya kuangalia na kufanya -Waeleweshe wanafunzi jinsi ya kuripoti watakachokiona 	<ul style="list-style-type: none"> -Matumizi zaidi ya mlango mmoja wa fahamu -Kuona zaidi ya kiicho wapeleka -mwalimu hapata unafuu wa kuelezea vitu vigumu 	<ul style="list-style-type: none"> Eneo zuri na linalofaa kwa shughuli huweza kuwa mbali na shule -Usimamizi wa wanafunzi huwa mgumu zaidi nje ya darasa - Wakati mwingine sehemu huwa hatarishi

Jedwali 3: Taratibu/mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, thamani na matumizi yake

Taratibu/mbinu	Ujuzi/thamani watakayoipata wanafunzi	Lini mwalimu anaweza kutumia utaratibu/mbinu hii
Majadiliano	<ul style="list-style-type: none"> - Mbinu za utatuzi wa matatizo na changamoto - Ujuzi wa mawasiliano - Mbinu na ujuzi wa kuripoti 	Mwanafunzi anapokuwa anaelewa kitu kuhusu dhana
Drama	<ul style="list-style-type: none"> - Wanafunzi hupata ujuzi wa kujieleza - Mwanafunzi huweza kujiamini zaidi 	Dhana inayohusu mabadiliko ya mwelekeo
Maonyesho	<ul style="list-style-type: none"> - Kipaji cha kutunga/kubuni - Ujuzi wa kujieleza 	Wakati wanafunzi wametengeneza vitu mbalimbali
Uwasilishi		
Kazi ya vikundi	<ul style="list-style-type: none"> - Kupata fursa ya kushikiana mawazo - Kupata ujuzi wa kuripoti 	<ul style="list-style-type: none"> - Hufaa zaidi kwa darasa kubwa - Mwalimu anapokuwa na vitu vingi vya kufundisha
Ugunduzi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuangalia • Usikivu • Utatuzi wa suala/ changamoto • Kuripoti 	Mwalimu anapotaka wanafunzi wagundue ukweli wenyewe
Maonyesho kwa vitendo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuangalia • Kujieleza • Matumizi ya njia za fahamu • Uchambuzi wa changamoto 	Mwalimu anapokuwa hana zana kwa wanafunzi wote

Shughuli za kufanya;

1. Kama shule ina mradi wa maji, tafuta mbinu / taratibu 3 ambazo zinaweza kutumika kuwafanya wanafunzi waweze kushiriki
2. Je unadhani mbinu ya drama inawezaje kupeleka ujumbe wa elimu ya mazingira hadi nje ya mazingira ya shule?

MATUMIZI YA ZANA ZA ELIMU YA MAZINGIRA

Utangulizi: Eneo hili litaonyesha jinsi gani wanafunzi wanaweza kutumia zana mbalimbali katika ufundishaji wa elimu ya mazingira. Wanafunzi watajifunza jinsi na wapi pa kutunza hizi zana.

Lengo: Kuongeza uwezo wa mwalimu wa kutumia zana anuwai za elimu ya mazingira katika ufundishaji

Hadi mwisho wa kitengo hiki wanafunzi wataweza

- Kutambua zana za elimu ya mazingira (EE materials) zilizopo
- Kuainisha maeneo katika mtaala ambako zana za elimu ya mazingira zinaweza kutumika
- Kueleza zana za elimu ya mazingira zinaweza kupatikana wapi?
- Kuelezea jinsi ya kuhifadhi hizi zana
- Kuweza kutumia zana za elimu ya mazingira katika kufundishia

Vifaa vya kufundishia elimu ya mazingira (EE materials)

- Ni nini?
- Vinapatikana wapi?
- Uhifadhi wake

Wanafunzi katika vikundi wajadili:

- Vifaa vya kufundishia elimu ya mazingira ni vipi? Wakae katika vikundi na waulize na waandike
- Majibu yatakayopatikana yaandikwe ili washiriki wote wafahamu kilichojiri
- Majibu yalinganishwe na jibu linalofuata

Vifaa vya elimu ya mazingira ni:

- Vifaa ambavyo vinawafanya watu kupata welewa wa mazingira na changamoto zake
- Kupata uzoefu na welewa wa mazingira na matatizo yake
- Kugundua thamani ya mazingira na motisha ya kulinda na kuendeleza mazingira
- Kupata ujuzi wa kugundua na kutatua changamoto za mazingira
- Kupata fursa za kuhusishwa kikamilifu katika kutatua matatizo ya mazingira

Vifaa vya elimu ya mazingira vinaweza kuwa katika mfumo wa:

- T-shirt
- Mabango
- Vipeperushi
- Vijitabu



- Kalenda
- Kofia n.k. fikiria na vingine zaidi

Uhifadhi:

Je mnaelewaje maana ya uhifadhi wa vifaa vya elimu ya mazingira? Walimu wanatunzaje / wanahifadhi vipi vifaa vya elimu ya mazingira katika shule zao na madarasani? Vifaa vya elimu ya mazingira sio vitabu. Ni vema vifaa hivi vikahifadhiwa sehemu ambayo ni salama, hali ya hewa inayofaa, pasafi na sehemu isiyo na mchwa, wadudu na panya.

Vifaa vinaweza kuhifadhiwa

- Kabatini
- Makasha ambayo hali ya hewa haitadhuru
- Plastiki
- Sehemu isiyo na vumbi

Upatikanaji wa Vifaa Vya Elimu ya Mazingira

Washiriki wafikirie ni wapi wanaweza kupata vifaa hivi ikichukuliwa kuwa vifaa vya elimu ya mazingira sio vitabu.

Mfano wa sehemu hizo ni:

- Maktaba za NEMC
- Taasisi ya ukuzaji mitaala
- Mitandao (internet)
- Mashirika/Taasisi mfano TFCG, EAMCEF, TAFORI

Matumizi ya Vifaa vya Elimu ya Mazingira

Mada za elimu ya mazingira zimeingizwa katika masomo ya shule za msingi. Vifaa vya elimu ya mazingira vinaweza kutumika katika masomo yote ya shule za msingi.

3. UBORESHAJI MTAALA

Uingizaji wa Elimu ya Mazingira katika mtaala

Utangulizi: Elimu ya mazingira inapata umaarufu katika sekta ya elimu katika nchi nyingi duniani. Vichocheo vinavyoleta maendeleo haya vinatofautiana kutokana na hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Lengo: Eneo hili linategemea kuangalia maana, malengo, kanuni, na uhusiano na sekta nyingine za elimu ya mazingira.

Uwezo: Baada ya mafunzo haya mwalimu ataweza:

- Kueleza maana ya elimu ya mazingira
- Kutambua na kuainisha malengo, na kanuni za elimu ya mazingira
- Kuelezea mtambuka (inter-disiplinary) wa elimu ya mazingira
- Elezea umuhimu wa elimu ya mazingira katika jamii yetu

Taratibu sahihi zinazofaa anazoweza kutumia mwalimu/mkufunzi

- Majadiliano
- Kazi za vikundi
- Tathmini ya mazingira
- Mihadhara
- Sinema

Changamoto za ufundishaji wa Elimu ya Mazingira katika mtaala katika nchi zinazoendelea

- Kimataifa, mataifa chini ya robo ndiyo yameingiza Elimu ya mazingira katika mitaala. Nchi ambazo zinaendelea bado Elimu ya mazingira haijapata uzito wa kuingizwa katika mtaala
- Fedha za kuendeshea shughuli hii ni kidogo
- Fedha kidogo katika uingizaji wa Elimu ya mazingira katika mtaala zimechangia pia kuwepo na miundo mbinu isiyokidhi, na hivyo walimu na wanafunzi kukosa motisha
- Mafunzo kidogo ya elimu ya mazingira. Katika nchi zinazoendelea ni walimu wachache sana ambao wamepata mafunzo ya elimu ya mazingira.

Maeneo ya mtaala ambayo yanafaa kuingizwa Elimu ya Mazingira

- Kamati ya shule
- Shughuli zinazoambatana na mtaala k.m muziki, dansi, drama, michezo
- Shughuli za nje ya shule k.m shule kutembeleana, safari za mafunzo, kazi za nje
- Ushirikiano kati ya shule na jamii
- Shughuli za shule za kila siku k.m baraza, sala
- Vipindi vilivyoko katika mtaala na muhtasari

- Klabu mbalimbali

Mtazamo wa Haki Sawa na Shule inayojali Mazingira (Rights-Based Approach and Eco-Schools)

Mfumo wa HAKI SAWA unaweza kuelezewa katika hatua saba za kuunda Shule inayojali Mazingira

Utangulizi: Hatua hizi saba zinatambuliwa kimataifa, hata hivyo mpangilio na jinsi ya kuzitumia hutegemea na eneo lenyewe.

Kuunda kamati ya Eco- School. Kamati hii inaundwa na wajumbe 11:

- Mwakilishi 1 kutoka Kamati ya Shule
- Mwakilishi 1 kutoka muungano/ushirikiano wa wazazi na walimu
- Wawakilishi 2 wa wazazi
- Walimu 2; mmoja wa kike na mwingine mwanamume
- Wanafunzi 4; wawili wasichana na wengine wavulana
- Mwalimu mkuu

Kamati inamhusu zaidi mwanafunzi. Wanafunzi wako katika hii kamati na inalenga zaidi wanafunzi kufanya kazi na wazazi, walimu na viongozi ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu bora.

Tathmini ya mazingira ya shule

Tathmini ya mazingira huangalia changamoto zilizoko shuleni kutokana na idadi, ubora, na upatikanaji wa rasilimali na athari za uharibifu wa mazingira shuleni na katika jamii, huangalia tabia na matendo ya watu na njia za kupatia kipato, uwekaji akiba/dunduiza na matumizi.

Tathmini ya mazingira huonyesha mahitaji, changamoto na matatizo ya wanafunzi kuhusiana na uendeleu wa mazingira na elimu bora ambayo shule na jamii kwa pamoja wanaweza kuyashughulikia. Tathmini huchanganua na kujua wanachostahili wanafunzi kupata kwa ajili ya kupata elimu bora na kujua mhusika/mtoaaji ni nani. Yale yote yatakayojitokeza katika tathmini yatatatua; haki kwa wanafunzi wote, matokeo ya ujifunzaji bora, kufundisha na kujifunza ambako ni sahihi na wenye kujibu mahitaji, ufundishaji na mbinu za ujifunzaji zinazomlenga/mhusisha mwanafunzi, motisha ya walimu na inayolinda jamii.

Kutengeneza maono na malengo

Katika hatua hii tunapata maandiko malumu yanayoelezea shule itakavyoshughulikia changamoto na matatizo yaliyogundulika wakati wa ukaguzi wa mazingira. Maandiko maalum haya, hukazia zaidi ubora wa elimu na ujumbe wake hutumika kuelezea haki na wajibu wa welewa ambao utaleta mabadiliko ya tabia ambayo yatachangia wanafunzi kupata elimu bora na mazingira endelevu. Haya yote huendelezwa na wanafunzi wenyewe ambayo huwajengeya uwezo wa kuwa viongozi, kufikiri kwa makini na kuweza kutatua matatizo/changamoto wanazokutana nazo.

Kutengeneza Mpango Kazi

Mpango Kazi huorodhesha shughuli, hatua za kuchukua, nani mhusika na muda wa kufanya shughuli husika, huongoza utekelezaji wa shughuli zilizopangwa, huwezesha kutekeleza malengo na ni zana/kifaa cha kupimia uwajibikaji. Mpango Kazi huonyesha haki ya mwanafunzi katika ushiriki wa kutoa maamuzi, masuala yanayohitajika kwa ajili ya kujenga

akili na mwili. Huonyesha shughuli za ujifunzaji kivitendo anazotakiwa afanye mwanafunzi na zana/vifaa venye uwezo wa kukuza elimu bora.

Kuhusisha mtaala (curriculum localization):

Hatua hii huhusisha matumizi ya mbinu/taratibu mahsusi za ufundishaji, hukazia matumizi ya zana zinazopatikana katika mazingira yetu na uwepo wa tathmini ya kila wakati (*continuous assessment*). Hatua hii inatakiwa itumiwe na walimu kuongeza welewa juu haki za binadamu, kuimarisha ufundishaji bora unaotumia mazingira ya shule, kuhusianisha ujifunzaji na ufundishaji unaotumia mazingira ya wanafunzi. Hatua hii huhakikisha kuwa mkazo unawekwa katika IVAC, mwanafunzi anakuwa mhusika mkuu katika mbinu za ujifunzaji na ufundishaji, ushirikishwaji wake unapewa kipaumbele kwa ajili ya kupata elimu bora baada ya kuboresha mbinu/taratibu za kujifunzia na kufundishia.

Ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Shule inayojali Mazingira (*Eco-school*)

Ufuatiliaji na tathmini hupitia na kuangalia maendeleo ya program, huandika maendeleo yaliyofikiwa na changamoto za program, kuna kutembelea mara kwa mara shughuli za program na kuchanganua/chunguza mpango kazi, shughuli baada ya shughuli kutathmini matokeo ya programu kwa walengwa na kuhusisha/kuingiza matokeo ya tathmini katika shughuli za programu. Hatua hii hutumia vipengele vya haki za binadamu kupima na kuorodhesha yale mazuri yaliyoonekana kwa ajili ya sera kuwajengea wanafunzi uwezo na kushiriki katika kudai haki zao za uwajibikaji, kutambuliwa, usalama, na uwajibikaji wa wazazi, walimu na viongozi. Hii itajenga mfumo wa uwajibikaji, ubora, ushiriki na utoaji maamuzi.

Kujulisha na kuhusisha:

Wazazi na viongozi katika jamii wana nafasi kubwa ya kufanya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu bora. Ushirikiano wao ni muhimu sana katika kutoa mazingira mazuri ya kusaidia shule ili iweze kuwa na uhusiano mzuri na jamii. Wanafunzi wanaweza kuhabarisha jamii kwa kutumia mbinu anuwai kama:

- Barua pepe
- Mbao za matangazo
- Redio
- Mabaraza
- Mikutano
- Ripoti za shule
- Muziki
- Drama
- Siku za wazazi (*open days*)

Njia hizi huwafanya wanafunzi kuongeza na kutumia ujuzi wa aina mbalimbali ambao huwafanya kupata haki ya njia stahiki kwa ajili ya elimu bora.

Shughuli:

1. Andaa mjadala kuhusu imani na thamani waliyo nayo jamii inavyoathiri mazingira
2. Andika wimbo, shairi au hadithi juu ya mazingira kwa ajili ya wanafunzi wa shule ya msingi

Uingizaji Miradi Midogo katika mtaala

Katika eneo hili mwanafunzi atawezeshwa kuelewa maana ya miradi midogo, kwa nini ni muhimu shuleni, inawezaje kutumiwa wakati wa mafunzo darasani, na wapi inaweza kuingizwa katika mtaala.

Matokeo ya ujifunzaji: Kipengele hiki kinatarajiwa kunoa uwezo wa mwanafunzi kuweza kutambua na kuchagua miradi midogo inayofaa kutumiwa katika mtaala

Uwezo: Hadi mwisho wa mafunzo haya mwanafunzi ataweza:

- Kuelezea miradi midogo ni nini?
- Kutambua miradi midogo ambayo inawezekana kutekeleza
- Kuchagua miradi midogo inayofaa kutekelezwa shuleni
- Kuelezea thamani ya miradi midogo kama njia ya kufundishia na kujifunzia
- Kutumia miradi midogo wakati wa mafunzo ya kawaida darasani
- Kutambua maeneo yanayofaa katika mtaala wa shule kuingizia miradi midogo

Maana ya Miradi Midogo

Miradi midogo ni majaribio na maonyesho madogo katika fani/somo rasmi na shughuli isiyo ya somo katika mazingira inayotekelezwa na wanafunzi ili iwafanye kuelewa vema zaidi na kutengeneza stadi za maisha.

Umuhimu wa Miradi Midogo shuleni

Miradi midogo shuleni ni muhimu kwa sababu:

- Huwafanya wanafunzi kupata maarifa na kuendeleza uwezo katika fani husika
- Huwafanya wanafunzi kushiriki na kuhusishwa katika mchakato wa kujifunza na ufundishaji
- Wanafunzi huweza kuendeleza ujunzi kimaisha kama kufikiri kwa makini wakati wakitekeleza miradi hii
- Miradi mingine ni njia za kuongeza kipato kama miradi ya kilimo ambayo huwa na kuuza mazao
- Wanafunzi huweza kuthamini faida za kufanya kwa vitendo na kuendeleza mawazo sahihi
- Inakuza ushirikiano wa shule na jamii
- Wanafunzi huelewa dhana sahihi zaidi kwa kushiriki moja kwa moja katika miradi
- Mifano ya miradi midogo ni pamoja na;
 - Upandaji miti
 - Ufugaji samaki
 - Kilimo cha bustani

Uchaguzi wa miradi-midogo

Mwalimu anatakiwa azielewe barabara dhamira/wazo (themes) na kuamua inayohitajika zaidi kufundishwa katika muhula na hivyo kuamua aina ya mradi utakaotekelezwa muhula huo.

Kwa mfano:

Darasa la tano; Jiografia; upandaji wa miti utasaidia katika dhamira ya kujifunza na ufundishaji ya mada hii ya 4.0 Kutegemeana katika Mazingira; Mada ndogo 4.3; Njia bora za kutunza mazingira.

Darasa la sita: Jiografia: 2.0 Shughuli za kiuchumi na athari zake katika mazingira: Mada ndogo: 2.4 Misitu

Shughuli zinazopendekezwa ni pamoja na:

- upandaji miti na nyasi katika eneo la shule na nyumbani
- utengenezaji wa vitalu vya miti
- kulinganisha misitu ya asili na ya kupandwa

Miradi midogo ya *Upandaji miti na Kilimo cha bustani* inafaa kuchaguliwa kwa shughuli hizi. Miradi ambayo inaweza kusaidia ujifunzaji wa mada moja au zaidi katika masomo ya shule kwa kipindi kimoja inafaa zaidi. Miradi hii itawawezesha wanafunzi kuona uhusiano uliopo katika masomo mbalimbali.

Matumizi ya miradi midogo katika kufundishia na kujifunzia

- Matumizi ya miradi midogo kwa kutumia taratibu/mbinu sahihi
- Miradi midogo shuleni inatekelezwa na kueleweka kwa kutumia njia za matendo za kujifunzia na kufundishia ambazo huhitaji ushiriki wa moja kwa moja wa wanafunzi wakiongozwa na walimu.

Taratibu/mbinu sahihi za kujifunzia /kufundishia:

Mbinu hizo ni pamoja na

- Maonyesho hasa majaribio na michakato
- Maelezo ya mchakato
- Utafiti na uchuguzi wa mchakato na shughuli huwa na mabadiliko baada ya muda
- Majadiliano katika vikundi
- Bungua bongo katika mambo muhimu juu ya miradi midogo
- Safari za mafunzo katika maeneo ya mradi na ya shule.

Uingizaji na Matumizi ya Miradi Midogo katika andalio la somo

Mfano wa andalio la somo

Uingizaji wa miradi midogo katika andalio la somo – (Viumbe Hai)

Darasa la nne: Sayansi

Tarehe	Somo	Darasa	Vipindi	Muda	Idadi ya wanafunzi

UJUZI:

LENGO KUU:

MADA KUU: Hifadhi ya maji na Udongo

MADA NDOGO: Mbinu mbalimbali za kuhifadhi maji na udongo shambani

MALENGO MAHSUSI: Kujua nmna matone ya mvua yanavyo sababisha mmomonyoko na jinsi mbolea ya samadi inavyo badilisha sifa ya udongo ya kuhifadhi maji


ZANA/VIFAA: Samadi, na shamba la migomba


REJEA: Michoro ndani ya boksi linalofuata

SOMO: 1. Kuchunguza kama mimea inayotambaa na majani mapana inaweza ku zuia mmomonyoko wa udongo.
2 Sifa za udongo na hifadhi ya maji


Vifaa: Mimea ya Migomba, Maharage, samadi

Njia: Mradi wa kilimo cha migomba kilicho changanywa na maharage na kutumia mbolea ya samadi.







Hifadhi ya maji shambani



Matone ya mvua inavyo sababisha mmomonyoko wa udongo



Majani ya migomba na maharage inavyozuia mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na kasi ya matone ya mvua



Mbolea ya samadi kuongeza uwezo wa udongo kuhifadhi maji kwa kubadilisha umbile la chembechembe za udongo

Uwezo: Mwisho wa kipindi hiki mwanafunzi aweze:

- Kuorodhesha mahitaji muhimu kwa uhai na ukuaji wa wanyama
- Kuonyesha faida ya kila aina ya mahitaji kwa uhai na ukuaji wa wanyama
- Kufanya majaribio kubaini umuhimu wa mahitaji ya wanyama kwa uhai na ukuaji wao
- Kuripoti matokeo ya ugunduzi wake

Taratibu/mbinu: kazi ya vikundi, maonyesho, kuangalia, kuweka rekodi na kuripoti

Mtiririko/mpangilio wa somo:

Kipindi hiki kitakuwa mojawapo ya vipindi vilivyopangwa kwa ajili ya dhamira (theme). Sehemu kubwa ya kazi kwa vitendo itafanyika nje ya muda wa darasani, lakini wakati wa kipindi mwalimu atapanga safari ya mafunzo katika eneo la mradi ili darasa waweze kuona:

- Mabadiliko/maendeleo yoyote
- Kujadili na mwalimu aongeze nyama
- Kutengeneza njia ya kwenda mbele

Wakati wote wa maelekezo darasa lielekezwe zaidi katika mradi mdogo

Shughuli za kufanya:

Angalia tena mtaala wa shule yako na uchague mradi mdogo unaofaa katika muhula na darasa utakalochagua

Eleza umuhimu wa Mradi Mdogo huo kwa darasa

Katika karatasi andika:

- Shughuli mbalimbali ambazo utawafanyisha wanafunzi wakati wa Mradi Mdogo
- Vifaa/zana utakazotumia katika kila hatua ya utekelezaji wa Mradi Mdogo
- Watu utakaowahitaji katika utekelezaji katika kila hatua ya Mradi Mdogo

4. USHIRIKIANO KATI YA JAMII NA SHULE

Kufahamisha/pasha habari na kuhusisha

Kuhusisha na kupasha habari kutahusu ushiriki wa jamii katika msaada wa kiufundi. Kitengo hiki kitaonyesha mbinu na jinsi jamii itakavyoshiriki katika miradi midogo inayohusu elimu ya mazingira. Vile vile kitengo kitajitahidi kugundua njia za kujulisha jamii juu ya elimu ya mazingira.

Lengo la kujifunza: Mwanafunzi awapashe habari jamii na ahusishwe katika masuala ya elimu ya mazingira pamoja na jamii yake.

Uwezo:

- Uwezo wa kugundua miradi midogo ya mazingira inayoendelea katika jamii.
- Shiriki na kuchangia katika mkutano wa elimu ya mazingira.
- Shiriki katika maonyesho ya elimu ya mazingira.
- Imba au andika mashairi yanayoonyesha masuala ya mazingira.
- Chora mchoro au tengeneza bango linalotoa ujumbe wa mazingira.

Kuifahamisha jamii

Utangulizi: Jamii na watu wake ndio wadau wakuu wa masuala yanayohusu uhifadhi wa mazingira. Ni vema jamii na watu wake wakapewa habari sio tu za mazingira bali na njia za kuyahifadhi.

Njia za kuifahamisha jamii ni pamoja na:

- ✓ Mikutano
- ✓ Mabango
- ✓ Kutumia viongozi watoa maamuzi
- ✓ Maonyesho
- ✓ Miradi
- ✓ Kutumia wataalamu
- ✓ Wanafunzi
- ✓ Drama
- ✓ Vipeperushi

Jedwali 4: Njia za kuifahamisha jamii juu ya elimu ya mazingira

Kipengele	Nini cha kutumia	Nini kifanyike	Matokeo
Mikutano	<ul style="list-style-type: none"> - Barua za kuwajulisha - mahali pa kufanyia mkutano 	<ul style="list-style-type: none"> - Wajulishe wadau - kuwa na zana za kusaidia kupeleka habari - nukuu 	<ul style="list-style-type: none"> ✓ Julisha wadau ✓ Badilisha mwelekeo ✓ Badilika tabia
Mabango	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Vifaa vya kuandikia ▪ Mabango ▪ Watu wa kuyaweka mahali pake ▪ Rasilimali za kuyatengeneza ▪ Watu wa kuyatengeneza 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Kukubaliana na cha kuweka katika hayo mabango ▪ Kuyajaribisha ▪ Wadau wayapate ▪ Kuwaelewesha kilichoko katika mabango 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Mabango yaliyobandikwa ▪ Jamii yenye habari
Viongozi watoa maamuzi	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Wawepo watoa maamuzi ▪ Utayari wa kuhabarishwa ▪ Uwezo wa kuwahabarisha wengine 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Kupata habari ambayo intakiwa ipelekwe kwa jamii ▪ Rasilimali ziwepo za kuwafanya watoe habari ▪ Watoa maamuzi wahabarishwe katika mkutano au semina 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Jamii iliyohabarika ▪ Mabadiliko ya mwelekeo wa watoa maamuzi na jamii
Maonyesho	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Zana/vitu vya kuonyesha ▪ Rasilimali watu ya kuelezea 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Maandalizi ya cha kuonyesha 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Jamii iliyohabarika ▪ Mabadiliko ya mwelekeo
Mashairi	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Wanafunzi ▪ Mkufunzi 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Wanafunzi hufunzwa kupitia mashairi juu ya mazingira 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Jamii iliyohabarika kutokana na mashairi
Wataalamu	Mtu mwenye habari ya kutosha		<ul style="list-style-type: none"> ▪ Jamii iliyohabarika
Miradi	Miradi ya maonyesho k.m. vitalu vya miti	Maandalizi ya miradi yenye kutoa mafunzo	Habari kwa jamii kwa kuangalia
Wanafunzi	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Zana za kufundishia ▪ Walimu wa mazingira ▪ Wanafunzi 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Wafundishe wanafunzi juu ya elimu ya mazingira ▪ Wapatie wanafunzi kazi za kufanya 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Wanafunzi waliohabarika ▪ Ujumbe kusambaa zaidi
Vyombo vya habari	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Matangazo ▪ Rasilimali za matangazo 	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Mpangilio wa matangazo 	Habari ambayo imerushwa kwa kutumia redio

Maswali ya tafakari

- Ni jinsi gani jamii inaweza kuhabarishwa juu ya ujumbe wa elimu ya mazingira?
- Je jamii inawezaje kuchangia katika kutunza mazingira?
- Je jamii inawezaje kutoa msaada wa kitaalamu shuleni?
- Jamii inawezaje kuendeleza au kushiriki katika miradi iliyoanzishwa na shule?

Katika kupasha habari ni vizuri kukawepo na welewa wa yafuatayo:

- Ni nani wa kumpasha habari?
- Ni nini cha kuwaeleza?
- Ni jinsi gani habari itapelekwa?

Ujuzi na jinsi ya kushirikiana maarifa

Ujuzi unaotumika katika kushirikiana maarifa hutofautiana kwani hutegemea ni watu gani wanashirikiana maarifa. Mfano inawezekana ni kati ya wanafunzi na wanafunzi, wanafunzi na walimu, walimu na wazazi, wanafunzi na wazazi au walimu na wadau. Hata hivyo wote hao ambao wanashirikiana habari hawana budi kutumia ujuzi ufuatao:

- *Kusoma/kuandika:* Watu ambao wenye maarifa ya elimu ya mazingira na wanataka kushirikiana na wenzao wataandika na wale ambao wanahitaji maarifa hayo watayasoma.
- *Kusikiliza/kusema:* Mwenye uwezo katika elimu ya mazingira akiamua kushirikiana na wengine anaweza kuongea na watu watakapokuwa wanamsikiliza na kukawa na uwezekano wa kuenea au kusambaa
- *Kuonyesha/ maonyesho:* katika jamii anaweza kuwepo mtu ambaye ana ujumbe wa elimu ya mazingira. Akifanya kimatendo mbele ya jamii atakuwa anashirikiana na jamii hata kama haongei. Anaishi kwa mifano.

Shughuli ya kufanya

- Kama unahitaji kumtumia mtaalamu wa elimu ya mazingira ni hatua gani za kufanya ili umpate?
- Kama unataka kufanya onyesho je utaihusisha vipi jamii?

Kuhamasisha ukusanyaji / uwekaji pamoja rasilimali

Lengo: lengo la kitengo hiki ni kumfanya mwalimu apate welewa wa uhamasishaji wa rasilimali

Matokeo ya ujifunzaji: Hadi mwisho wa kitengo hiki mwalimu aweze:

- Kuonyesha stadi za kuhamasisha na kusimamia rasilimali ili kukuza elimu kwa maendeleo endelevu

Uwezo utokanao na ujifunzaji: Ifikapo mwisho wa kitengo hiki mwalimu aweze

- Kuelezea uhamasishaji na usimamizi wa rasilimali
- Aweze kufanya uhamasishaji rasilimali kwa matendo

- Aweze kufanya maamuzi sahihi kuhusu uhamasishaji na usimamizi wa rasilimali
- Aweze kuonyesha uwezo wa uhamasishaji na usimamizi wa rasilimali

Mbinu sahihi atakazotumia mwalimu ni pamoja na:

- Majadiliano
- Kutembelea na kukagua jamii
- Kazi za vikundi
- Mihadhara

Rasilimali ni nini? Rasilimali ni vitu/zana zilizoko kwa ajili ya shughuli lengwa. Rasilimali ni pamoja na watu, vifaa, mitambo na vinginevyo vinavyotumika katika kupanga, kutekeleza na kutathmini programu

Aina ya rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya ukuaji na utendaji wa taasisi ni:

- Rasilimali fedha
- Rasilimali watu
- Rasilimali maliasili

Maana ya Uhamasishaji wa rasilimali

Ina maana ya mchakato wa kukusanya rasilimali pamoja kama vile maarifa, fedha, vyombo vya habari, nguvukazi, umoja, uhalali, nguvu ya ndani na nje kwa njia ambayo ni madhubuti, endelevu, ya uwazi, sawasawa kwa ajili ya kukua na maendeleo chanya ya taasisi.

Kwa nini uhamasishaji wa rasilimali ni muhimu?

Ni muhimu na busara kutengeneza mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali kwani unaweza kukusaidia kutumia ulivyonavyo ukafanikiwa badala ya kuomba misaada toka nje. Ni vema ukatumia ulivyo navyo badala ya kungojea msaada kwani rasilimali zinazidi kupungua na ushindani katika kupata fedha za wafadhili unazidi kuwa mgumu duniani.

5. KUCHANGISHA FEDHA (FUNDRAISING)

Huu ni mchakato wa kukusanya michango/fedha za hiari au rasilimali nyingine kwa kuomba michango kwa watu na taasisi mbalimbali.

Kabla ya kuchangisha fedha, ni vema ukatengeneza mazingira ambayo yatawafanya wachangiaji wahamasike. Vipengele kadhaa vitakufanya ufanikiwe katika hili navyo ni:

- Onyesha wewe ni nani na unathamini vipi dira na dhima ya taasisi yako? Dhima yako ina uhusiano gani na jamii unayoitumikia?
- Hakikisha program yako ina matumaini ya kutoa matunda
- Onyesha kuwa ulishatenda yakakamilika
- Usimamizi na uongozi thabiti wa wafanyakazi wako ambao wataonyesha uwajibikaji na uwazi wa taasisi
- Usimamizi mzuri wa fedha utakaoweza kutunza zitakazochangishwa na kuonyesha uaminifu
- Kuwa na taswira nzuri
- Kuaminika katika kutegemeana na ushirikiano wa habari wenye tija kati ya taasisi na jamii na wadau wengine
- Uwezo wa kutafuta, kutengeneza na kuendeleza rasilimali mpya na hasa zilizoko katika jamii.

Utafiti unaohusu uchangishaji fedha

Uchangishaji fedha huhitaji maarifa ya juu ya hali halisi ya eneo unalotegemea kukusanya fedha lilivyo kwa mfano:

- Sheria za mahali hapo zikoje? Hasa kuhusiana na ukusanyaji fedha?
- Mfumo wa kodi unaweza kuathiri jinsi ya kuripoti mapato na ikafanya uchaguzi wa shughuli za kufanya wakati wa kuchangisha fedha
- Njia ambazo zilitumiwa na taasisi nyingine zinaweza kusaidia katika zoezi zima
- Kuegemea katika utamaduni, imani, desturi za mahalilengwa inaweza kuongeza idadi ya wachangiaji

Rasilimali/mali za jamii

Kabla ya kuchangisha fedha ni vema kugundua rasilimali (fedha na zisizo fedha) za mtu mmoja mmoja, jamii, taasisi zisizo za serikali na vikundi. Rasilimali ambazo si za kifedha ni pamoja na ujuzi, vipaji na uwezo. Kugudua rasilimali hizi katika jamii kutasaidia kubuni njia mbadala na rasilimali zenye ufanisi zaidi.

Watu wa kujitolea

Watu wa kujitolea wanaweza kuchangia katika rasilimali na taasisi ikanufaika sana. Kabla ya kuwahusisha ni vema ukajua motisha na mategemeo yao. Watu wa kujitolea wanaweza kuwa wastaafu, vijana, wataalamu, wanafunzi. Wanaweza kuwa Watanzania au wa kutoka nje ya nchi. Unaweza kupata kitu kikubwa sana kutoka kwa watu wa kujitolea. Kabla ya kuwachukua angalia yafuatayo:

- Angalia shughuli inayohitajika kufanyika, muda wa kujitolea, na sifa/ujuzi unaohitajika
- Kutegemea na mahitaji tafuta watu wa kujitolea kutoka shule, vyuo, vyuo vikuu, au kutoka nje ya nchi, mashirika, serikalini.
- Kuhakikisha ubora wa kazi ni vema kuwafanyia usaili (interview), chagua na kuwapata wenye sifa zinazohitajika na kuwapa kazi ya kufanya
- Wahifadhi na kuwatumia watu wa kujitolea na hakikisha wanapata mwongozo jinsi ya kufanya kazi, wapatie mafunzo pale inapobidi ili kuongeza ufanisi kazini
- Watambue watu hawa katika mikutano, na jamii

Uongozi na majukumu katika uhamasishaji wa rasilimali

Utawala imara kwa mfano, bodi ya wakurugenzi ni muhimu kwa usimamizi wa taasisi katika juhudi za uhamasishaji wa rasilimali, wafadhili mara nyingi huulizia juu ya hii bodi kama ipo au hapana. Bodi hii huundwa na watu wa kujitolea wenye ujuzi Fulani, maarifa na uzoefu. Hawa ndio wawajibikaji wa kwa waliotoa/changia rasilimali.

Miradi ya kuongeza kipato

Michango kutoka kwa wanachama

Matukio muhimu: Matukio muhimu ni sehemu nzuri ya kuweza kuchangisha fedha. Unaweza kuuza tiketi kwa ajili ya tukio, dansi, sinema au michezo, na ukaongeza kafaida kidogo katika hizo tiketi. Unaweza kuuza t-shirt zenye nembo ya taasisi, chakula, au michoro.

Uthubutu wa biashara (business venture): Unaweza kuwatoza wanaohudhuria warsha, au unaweza kuuza vyakula kutoka bustani ya mboga n.k

Kabla ya kuingia katika biashara ni vizuri kufanya utafiti juu ya hiyo aina ya biashara.

Utafiti huo ujaribu kuona:

- Shughuli za kuleta faida ambazo zinaruhusiwa kufanywa na taasisi husika kisheria
- Uhusiano uliopo kati ya dhima ya taasisi na biashara yenyewe
- Nini malengo ya biashara?
- Je soko lipo la kitakachozalishwa na biashara lengwa?
- Umemtambua mlaji wa biashara lengwa?
- Ni vitu gani kitaifa, kimataifa au kijamii ambavyo vinaweza kuathiri biashara lengwa?
- Ushindani ukoje kutoka kwa mashirika na taasisi nyingine?

Kutengeneza mpango wa biashara

- Onyesha uwezo wa taasisi
- Jinsi utakavyofanya biashara

- Ni nani atakayesimamia hiyo biashara?
- Mtaji wa kuanzisha biashara, gharama za kila mwezi, na hasara na faida zinazotegemewa

Angalizo: Shughuli ya biashara inahitaji ujuzi maalum katika fani ya uhasibu, usimamizi wa fedha, masoko, usimamizi wa watu, na uthibiti ubora.

Maeneo mengine ambayo yanaweza kutoa msaada kifedha kwa ajili ya maendeleo ya miradi

- Mifuko kwa mfano EAMCEF iliyoko Morogoro
- Watu binafsi
- Mashirika
- Mashirika ya dini
- Serikali,
- Ofisi za balozi mbalimbali
- Klabu mfano rotary clubs, Lions club

Mara nyingi watoa fedha huwa na mpangilio wao wa kuomba hizo fedha. Mfano

Jedwali 5: Mpangilio wa kuomba ufadhili

Mawasiliano	Jina la mhusika, anwani ya taasisi, barua pepe, simu.
Muhtasari	Muhtasari wa andiko, na lengo la na kwa nini fedha zinahitajika
Muktadha	Maelezo ya matatizo yanayoiathiri jamii, na kwa nini mradi ni muhimu
Maelezo ya mradi	Jinsi ya kutekeleza mradi; yakiwepo malengo, shughuli, walengwa, matokeo, muda, wadau wengine
Ufuatiliaji na tathmini	Jinsi mradi utakavyofuatiwa na kupimwa
Bajeti	Gharama ya mradi, iliyoombwa, mtakachochangia, na vyanzo vingine
Habari ya Taasisi	Utangulizi, muundo wa utawala, dhima ya taasisi, ujuzi na uwezo wa wafanyakazi, n.k.

Faharasa

Anuwai: aina mbalimbali au tofauti.

Bioanuwai: mfumo kamili wa maisha duniani pamoja na uwiano wa asili wa michakato na miingiliano ambayo inaudumisha

Chanzo cha Maji: eneo ambalo maji ya mvua hujikusanya na kuelekea katika mito na hifadhi nyingine za maji.

Elimu bora na endelevu: ni ile inayomtayarisha mwanafunzi kujifunza kwa kuonisha elimu aipatayo shuleni na maisha yake ya kila siku akishirikiana na jamii inayomzunguka. Aidha ni ile inayomwezesha mwanafunzi kujenga dhana ya ubunifu, kuweza kuchanganua matatizo na mbinu za kuyatatua.

Elimu ya mazingira: ni elimu inayomwezesha binadamu kupata maarifa, stadi, mwelekeo na maadili ambayo yatamsaidia kuyaelewa mazingira yake na kutumia rasilimali zilizopo kumpatia mahitaji yake na maendeleo endelevu

Maendeleo: Kwa ufupi maendeleo ni ustawi wa maisha ya watu. Kwa maana kwamba, watu wapate mahitaji muhimu ya kuishi kama chakula bora, maji, huduma bora za afya, malazi, elimu na huduma nyingine za kijamii.

Maendeleo endelevu: Ili jamii iwe na maendeleo endelevu inahitaji kukidhi mahitaji ya sasa bila kuharibu au kuzuia vizazi vijavyo kupata na kukidhi mahitaji yao muhimu. Ni falsafa ya namna tunavyoweza kutumia rasilimali zinazotuzunguka na kuhakikisha tunawarithisha watoto wetu rasilimali hizo bila kuzimaliza ili nao waweze kuendeleza maisha yao

Mahitaji muhimu: Ni vitu ambavyo binadamu anavihitaji kutoka katika mazingira yake ili aweze kuishi

Maliasili: vitu vinavyotokana na mazingira ambavyo vina manufaa na thamani, mfano misitu, madini, maji na kadhalika.

Mazingira: vitu vinavyomzunguka binadamu, wanyama na mimea na uwiano baina yao

Rasilimali: Rasilimali ni vitu/zana zilizoko kwa ajili ya shughuli lengwa. Rasilimali ni pamoja na watu, vifaa, mitambo na vinginevyo vinavyotumika katika kupanga, kutekeleza na kutathmini programu

Uhifadhi wa Maliasili: kulinda maliasili na kuhakikisha mali hizo hazitumiwi vibaya au kuharibiwa au kupotezwa ili tuweze kuendelea kuishi katika mazingira mazuri.

ORODHA YA KUPIMIA ECO-SCHOOLS KWA AJILI YA BENDERA YA KIJANI

KAMATI YA ECO-SCHOOLS

Je shule yako inayo Kamati ya Eco-schools ambayo hukutana angalau mara sita kwa mwaka?

Je wanafunzi wanahusishwa katika majukumu ya kuendeleza Kamati?

Je Kamati ya Eco-schools shuleni kwako ina wajumbe wanaotokana na wazazi?

TATHMINI YA MAZINGIRA

Je Kamati ya Eco-schools imefanya na kukamilisha Tathmini ya Mazingira ambayo imehusisha mada husika? Je Kamati imewasilisha matokeo ya Tathmini na kuiandikia ripoti?

Je wanafunzi walihusika katika kufanya Tathmini ya Mazingira?

Je Kamati ya Eco-schools imeyajadili matokeo ya Tathmini ya Mazingira na kuyawasilisha kwa jumuiya kubwa ya shule?

MPANGO KAZI

Je Kamati ya Eco-schools imeandaa Mpango Kazi uliokamilika?

Je Mpango Kazi ulioandaliwa umeweka kipimo cha muda? Nani mhusika na shughuli zitafuatiliwaje pamoja na kupimwa?

Je Kamati ya Eco-schools imewasilisha Mpango Kazi kwa jumuiya yote ya shule?

Hakikisha kuwa wanafunzi wanahusishwa katika kutengeneza Mpango Kazi.

KUHUSISHA MTAALA

Je uendelevu umeonyeshwa angalau katika maeneo 3 ya mtaala?

Je uendelevu wa mfumo wa Eco-schools ulihusishwa katika mtaala wa shule wakati wa uandaaji?

KUJULISHA NA KUHUSISHA SHULE NZIMA NA JAMII

Je shule ina mbao za matangazo ambazo zinaonyesha kwa uwazi shughuli za Eco-schools?

Je Kamati ya Eco-schools huwasilisha shughuli zake mara kwa mara kwa shule na jamii? (kwa kutumia mikutano, magazeti, redio n.k)

Je shule imeshashirikisha shule nyingine zinazotaka kujiunga na program ya Eco-schools mafanikio ya shughuli za Eco-schools?

TATHMINI NA UPIMAJI

Je shule inao ushahidi wa kuonyesha maendeleo yake? Je shule imekusanya takwimu za kuonyesha maendeleo yake ?

Je takwimu zilizotokana na tathmini zimetumika katika kutengeneza na kutumika katika mtaala wa shule?

MAONO (ECO-CODE)

Je shule inayo maono yaliyokubalika na kuwekwa sehemu sahihi?

Je maono yanawekwa sehemu ambayo kila mwanafunzi na jaumuiya ya shule wataweza kuyaona?

Je maono (Eco-Code) yanajulikana na wanafunzi na jumuiya kubwa ya shule?

Kuhusu Shirika la Kuhifadhi misitu ya Asili Tanzania / Tanzania Forest Conservation Group

Kiongozi hiki kimetengenezwa na Shirika la Kuhifadhi misitu ya Asili Tanzania (TFCG).

TFCG ni shirika lisilo la kiserikali ambalo dhamira yake ni kuhifadhi na kurudisha bioanuwai ya misitu muhimu kidunia ya Tanzania kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijayo.

Program ya Shule inayojali Mazingira ilianzishwa 1994 kama program ya kimataifa kwa ajili ya elimu ya mazingira na usimamizi kwa lengo la kuongeza welewa wa wanafunzi juu ya masuala yahasuyo maendeleo endelevu kupitia mafunzo darasani pamoja na matendo shuleni na jamii.

Duniani program hii inatekelezwa na shule zipatazo 49,000 katika nchi 64, ikihusisha wanafunzi zaidi ya milioni 16, walimu zaidi ya milioni 1.2 na bendera za kijani zaidi ya 13, 301 zimekwishakutolewa.

Hapa Tanzania program ya Shule inayojali Mazingira ilianza 2015 kwa kushirikisha shule za msingi 20 wilayani Mvomero katika mkoa wa Morogoro

Programu ya Eco-schools Tanzania inafadhiliwa na serikali ya Denmark kupitia shirika la Danish Outdoor Council.